MAFUNZO YA WALIMU KAZINI NGAZI YA SHULE
KWA MWALIMU WA DARASA LA I-III

Moduli ya Kumi na Moja:

MSAMIATI

Mwongozo wa Mratibu wa Mafunzo ya Walimu Kazini Ngazi ya Shule

UKaid
from the British people

equip Tanzania
Education Quality Improvement Programme

Moduli hii imetayarishwa kwa ushirikiano na:

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi
Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
Taasisi ya Elimu Tanzania
Chuo Kikuu cha Dodoma
Chuo cha Ualimu Morogoro
Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam
Chuo Kikuu Huria cha Tanzania
Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa
EQUIP-Tanzania

Moduli hii imewezeshwa kwa ushirikiano na:

C.C.U Butimba
C.C.U Bustani
C.C.U Tabora
C.C.U Ndala
C.C.U Kasulu
C.C.U Kabanga
C.C.U Bunda
C.C.U Tarime
C.C.U Shinyanga
C.C.U Mpwapwa

DIBAJI

Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, imetoa kipaumbele katika sekta ya elimu ili kuleta mageuzi ya kiuchumi na kijamii. Lengo la Dira ya Maendeleo ni kuwa na taifa la watu waliolelimika na jamii iliyo tayari kujifunza kufikia 2025. Serikali ya Tanzania imethibitisha kwa vitendo kuwa Elimu ni kiambato muhimu katika kupunguza umaskini na kuimarisha maendeleo ya taifa. Kwa muda mrefu serikali imetambua kuwa "Ubora wa Elimu yoyote hauwezi kuwa bora kuliko mwalimu mwenyewe" hivyo imetilia mkazo mafunzo kazini kwa walimu kupitia mikakati mbalimbali ili kuimarisha umahiri wa walimu katika ufundishaji na ujifunzaji darasani.

Katika kuongeza ufanisi wa ufundishaji na ujifunzaji darasani, Taasisi ya Elimu Tanzania kwa kushirikiana na EQUIP-Tanzania, wameandaa moduli hii ambayo imesheheni kazi mbalimbali ambazo waalimu mtazitenda katika vikundi wakati wa mafunzo kwa kutumia mbinu ya Mafunzo ya Walimu Kazini ngazi ya shule. Mbinu hii inatambua umuhimu wa walimu kujifunza pamoja na kubaini changamoto zinazowakabili ili kupata suluhisho la changamoto za ufundishaji na ujifunzaji kwa pamoja.

Moduli hii ya Mafunzo ya Walimu Kazini, imeandaliwa ili kusaidia juhudi za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kuhakikisha kuwa mbinu fanisi zinatumika darasani wakati wa ufundishaji na ujifunzaji. Moduli hii pia inawasaidia walimu kushirikishana uzoefu na umahiri katika ufundishaji na ujifunzaji darasani. Vilevile Moduli inatoa mafunzo ya ziada ikitarajiwa kuwa walimu watakuwa wamekwisha pata Mafunzo Kabilishi ya utekelezaji wa Mtaala ulioboreshwa wa kuimarisha ufundishaji wa KKK kwa wanafunzi wa darasa la kwanza na la pili.

Taasisi ya Elimu Tanzania inatarajia kuwa moduli hii itawasaidia walimu kuimarisha umahiri wa ufundishaji na ujifunzaji ili kuwasaidia wanafunzi waweze kujenga uwezo unaokusudiwa wakati wa kujifunza.

Changamoto iliyo mbele yetu ni kuhakikisha kuwa tunaonyesha kwa vitendo matokeo mazuri yanayotokana na maudhui ya moduli hii wakati wa ufundishaji na ujifunzaji darasani ili kuimarisha ubora wa elimu ya shule ya msingi.

Dr. Leonard Akwilapo
Kaimu Mkurugenzi Mkuu,
Taasisi ya Elimu Tanzania.

Maelezo Muhimu kwa Mratibu wa Mafunzo ya Walimu Kazini Ngazi ya Shule

Mwongozo huu utatumika sanjari na moduli ya kumi na moja ya mwalimu ili kumsaidia mratibu wa mafunzo kuwa na mpangilio mzuri wenye kufuata hatua kwa hatua ili kuwafanya walimu washiriki kikamilifu katika kujifunza maudhui ya moduli ya kumi na moja.

Mwongozo huu umegawanyika katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza ambayo ni upande wa kushoto wa mwongozo unabeba maelezo ambayo mratibu wa mafunzo ya walimu kazini ngazi ya shule atatakiwa kuyafuata wakati wa kuratibu kipindi cha kujifunza maudhui ya moduli. Sehemu ya pili ambayo ni upande wa kulia wa mwongozo unabeba maudhui yaliyo kwenye moduli ya mwalimu ambayo watayasoma wakati wa kipindi cha kujifunza.

Wakati wa kipindi cha kujifunza, unatakiwa kufuata maelezo yanayokuongoza yaliyo upande wa kushoto wa mwongozo huu na kuyahusianisha na maudhui yaliyo kwenye moduli ya mwalimu ambayo yapo upande wa kulia wa mwongozo huu kama yanavyosomeka kwenye moduli ya mwalimu.

MAELEKEZO NA TASWIRA KATIKA MODULI

Kuna picha na michoro mingi katika moduli. Baadhi zinajirudia mara nyingi kwa sababu zinamaanisha jambo mahususi linalotokea. Zifuatazo ni mifano ya taswira mbalimbali ambazo zinapatikana katika moduli pamoja na kile ambacho zinawakilisha:

Jadili na mwenzako: Wakati wote wa kusoma moduli, walimu wataelezwa kufanya kazi pamoja na mwalimu mwingine juu ya maswali au kazi.

Fikiri– Wawili wawili – Shirikishana: Kama ilivyo katika maelezo ya hapo juu, hapa vilevile walimu wanafanya kazi wakiwa wawili wawili. Japokuwa, hapa walimu wanatafakari mmoja mmoja kwanza juu ya swali au tatizo, halafu mwalimu anafanya kazi na mwenzake na mwishoni wanawasilisha katika kundi lote.

Jadiliana katika kikundi: Wakati mwingine walimu wataelekezwa kutafakari au kujadili maswali mbalimbali katika kikundi.

Soma: Katika kila moduli kuna "dhana kuu" ambayo kwa kawaida huwasilishwa kwa kirefu katika maelezo.

Andika: Moduli itawahamasisha walimu kuchukua maelezo na kuandika fikra zao na majibu.

Igizo: Baadhi ya mazoezi yatahitaji walimu kuigiza kazi ya KUFUNDISHA wakati wengine watapaswa kuigiza kama wanafunzi.

MAELEKEZO KWA MRATIBU WA MAFUNZO YA WALIMU KAZINI

Kabla ya kuanza moduli hii, angalia 'maelekezo muhimu' na hakikisha kuwa wewe na walimu mnayatekeleza.

Tafadhali waambie walimu wajiorodheshe na kusaini hapa chini.

Tarehe:	Shule:	Wilaya:	Mkoa:
Muda wa kuanza:	Jina la Mratibu na sahihi yake:		
Muda wa kumaliza:	Jina la Mwalimu Mkuu na sahihi yake:		

	JINA LA MWALIMU	ME / KE	SAHIHI:	DARASA
1				
2				
3				
4				
5				
6				
7				
8				

WAAMBIE WALIMU:

"Sasa tutasoma utangulizi wa moduli hii. Tutasoma matini kwa sauti na kwa kupokezana. Baada ya mwalimu wa kwanza kusoma aya ya kwanza, atamwita mwalimu mwingine kwa jina ili asome aya inayofuata."

MODULI YA 11: MSAMIATI

MAUDHUI YA MODULI

Moduli ya 5 – 8 inahusu dhana na mbinu za KUFUNDISHA kusoma ambazo zinaendana na mabadiliko yaliyo kwenye muhtasari mpya wa darasa la kwanza na la pili. Moduli hii pia inahusu baadhi ya dhana na shughuli kama zilivyoanishwa kwenye muhtasari mpya wa darasa la kwanza na la pili. Moduli hii inahusu **ukuzaji wa msamiati**, huu ni mchakato ambao wanafunzi wanajifunza na kutumia maneno mapya. Upanuzi wa msamiati wa wanafunzi utainua ufahamu wao wa kusoma; hata hivyo, kujifunza msamiati mpya kunahusisha mazoezi ya aina nyingi. Utafiti unaonesha kuwa wanafunzi wanahitaji kukutana na neno jipya walau mara saba (7) katika mazingira tofauti kabla hawajalikumbuka. Moduli hii itaanzisha mbinu mbalimbali za kuwafundisha wanafunzi maneno mapya.

DHANA KUU

1. **Msamiati wa kusikiliza na kuongea:** Ni maneno ambayo wanafunzi wanayabaini na kuelewa maana yake wakati wanapoyasikia au kuyataja. Wanafunzi wanaweza kujua neno kwa kulitamka, lakini wasiweze kulibaini ikiwa wataliona limeandikwa.
2. **Msamiati wa Kusoma na Kuandika:** Ni maneno ambayo wanafunzi wanabaini na kutambua maana zake wanapoyasoma au wakayaandika. Wanafunzi wanaweza kubaini neno, lakini wasipolijua maana yake, neno hilo linakuwa siyo sehemu ya msamiati wao wa kusoma na kuandika.
3. **Msamiati Kiini:** maneno ambayo yanaendana na mada fulani. Kwa mfano, msamiati kiini kwa ajili ya "shamba" unaweza kujumuisha: ghala, mnyama, ng'ombe, kuku, mkulima na bustani.

MALENGO YA MODULI

Mwisho wa moduli hii, walimu watakuwa na uwezo wa:

1. Kueleza umuhimu wa ukuzaji wa msamiati katika kuimarisha ufahamu
2. Kuwasaidia wanafunzi kuelewa maana ya maneno wanayosoma na kuwa na uwezo wa kujifunza kutoka kwenye neno wanaloliandika
3. Kutumia mbinu hizi kusaidia uwezo wa wanafunzi kujifunza maana za manneo wasiyoyafahamu na kujenga msamiati wao.
4. Kutengeneza "Kuta za maneno" na kadi za maneno ili kusaidia mbinu za ukuzaji wa msamiati

MAELEKEZO MUHIMU

Njoo na vitu vifuatavyo:

1. Moduli ya mafunzo ya walimu kazini na kalamu
2. Walau maneno 10 ambayo unafundisha kwenye kiwango chako
3. Viweka alama au mkaa
4. Karatasi 6 – 8 za ukubwa wa A4 za manila kwa kila mwalimu (kama hakuna kadi za manila, tumia karatasi iliyo wazi au bodikadi)
5. Karatasi zilizofomekwa (kama una Kivunge cha Kufundishia cha EQUIP-Tanzania)
6. Gundi ya karatasi

TARATIBU ZA KUJIFUNZA KWA KILA KIPINDI

1. Kutana katika sehemu tulivu yenye ubao kama inavyoonekana katika picha
2. Panga madawati/meza ili kuwezesha washiriki wote waonane na kuongea kwa pamoja
3. Waeleze walimu wawe huru kuuliza maswali kama hawajaelewa
4. Waeleze walimu kuwa msaada kwa wenzao
5. Waeleze walimu kuwa wabunifu na kufikiria dhana watakazojifunza na jinsi zitavyohusiana na darasa lao
6. Waeleze walimu waweke simu zao katika hali ya mtetemo

TAFAKARI

WAAMBIE WALIMU:

“Tangu moduli ya 10, mmefanyia mazoezi shughuli mbili kwenye kipindi cha kujifunza kusoma na kuandika. Orodhesha mafanikio mliyoyaona pamoja na changamoto mlizokabiliana nazo wakati wa KUFUNDISHA maudhui ya moduli hiyo darasani kwako. Una dakika 5 kwa ajili ya kazi hii.”

WAAMBIE WALIMU:

“Sasa tutajadili kwa pamoja mafanikio na changamoto katika kikundi. Kwa kila changamoto ambayo imewasilishwa tufikiri kwa pamoja kuhusu namna ya kukabiliana nayo. Kumbuka kuandika ufumbuzi ambao unaweza kukabiliana na changamoto zilizojitokeza. Tutatumia dakika 10 kwa majadiliano.”

TAFAKARI

Katika kipindi cha mwisho tulisoma kuhusu **misingi ya kuandika.** Orodhesha mafanikio uliyoyaona pamoja na changamoto ulizokabiliana nazo wakati wa KUFUNDISHA maudhui ya moduli hiyo darasani kwako.

ANDIKA PEKE YAKO (DAKIKA 5)
Tafadhali andika kwenye visanduku mafanikio na changamoto ulizokutana nazo wakati wa kutekeleza mikakati hii

Mafanikio
(Elezea utaratibu uliotumia na fafanua jinsi ulivyofanikiwa)

Changamoto
(Elezea utaratibu uliotumia na fafanua changamoto zake)

JADILIANA KATIKA KIKUNDI (DAKIKA 10)

1. Shirikisha wenzako kwenye kundi mojawapo kuhusu uzoefu huo.
2. Kwa kila changamoto, pendekeza namna ya kukabiliana nayo.
3. Wakati wa majadiliano, andika ufumbuzi unaoendana na changamoto ulizobainisha.

Njia Muhimu za Ufumbuzi
(Mawazo muhimu na mahususi kwa wenzetu)

UTANGULIZI

WAAMBIE WALIMU:

“Leo tutaanza na zoezi la kusoma. Ukiwa na mwenzako, soma sentensi ambazo unaziona na kisha fuata maelekezo yaliyoko chini ya kila sentensi. Baadhi ya maneno kwenye sentensi yataonekana kama mageni kwako. Hiyo ni sawa! Jaribu kujibu maswali kwa uwezo wa juu kadri utakavyoweza.”

(Waambie walimu watoe majibu yao baada ya kumaliza kujibu maswali matano)

“Sasa, ngoja tupitie majibu yenu. Tunafikiri ‘toku’ inamaanisha nini kwa kuzingatia sentensi pamoja na picha tuliyoona?”
Ruhusu walimu kutoa majibu yao, wengine wanaweza kuwa na majibu tofauti na wengine.

“Umejuaje?”
Kama walimu watakuwa na maana tofauti kuhusu neno ‘toku’, waambie wajadili na kutoa jibu lililosahihi. Jibu sahihi ni ‘shuleni’.

“Kwa kuzingatia sentensi na picha, unafikiri ‘gotuki’ inamaanisha nini?”
Ruhusu walimu kutoa majibu yao, wengine wanaweza kuwa na majibu tofauti na wengine.

“Umejuaje?”
Kama walimu watakuwa na maana tofauti kuhusu neno ‘gotuki’, waambie wajadili na kutoa jibu lililosahihi. Jibu sahihi ni ‘swali’.

“Ulisema ‘kukiki’ ina maanisha nini?”
Ruhusu walimu kutoa majibu yao, wengine wanaweza kuwa na majibu tofauti na wengine.

“Umejuaje?”
Kama walimu watakuwa na maana tofauti kuhusu neno ‘kukiki’, waambie wajadili na kutoa jibu lililosahihi. Jibu sahihi ni ‘kusoma’.

“Ulisema ‘bilabu’ inamaanisha nini?”
Ruhusu walimu kutoa majibu yao, wengine wanaweza kuwa na majibu tofauti na wengine.

“Umejuaje?”
Kama walimu watakuwa na maana tofauti kuhusu neno ‘bilabu’, waambie wajadili na kutoa jibu lililosahihi. Jibu sahihi ni ‘mwalimu’.

“Ulisema ‘wawati’ inamaanisha nini?”
Ruhusu walimu kutoa majibu yao, wengine wanaweza kuwa na majibu tofauti na wengine.

“Umejuaje?”
Kama walimu watakuwa na maana tofauti kuhusu neno ‘wawati’, waambie wajadili na kutoa jibu lililosahihi. Jibu sahihi ni ‘sauti’.

UTANGULIZI

ZOEZI LA KUCHANGAMSHA (DAKIKA 10)

Kwa kushirikiana na mwenzako, soma maneno kwenye sentensi zinazofuata na fuata maelekezo. Baadhi ya maneno yatakuwa mageni kwako. Hiyo ni sawa! Jaribu kujibu mas wali kwa namna utakavyoweza kwa uwezo wako wote.

Kwa kushirikiana na mwenzako, soma maneno kwenye sentensi zinazofuata na fuata maelekezo. Baadhi ya maneno yatakuwa mageni kwako. Hiyo ni sawa! Jaribu kujibu maswali kwa namna utakavyoweza kwa uwezo wako wote.

Leo, nilienda toku kujifunza kukiki vitabu.
Bilabu wangu aliniuliza gotuki kuhusu wawati ya herufi.

1. Zungushia maneno ambayo ni mageni kwako.
2. Halafu angalia kwenye picha hizi hapa chini kujifunza baadhi ya maneno mageni kwako yana maana gani.
3. Kwa yale maneno yasiyo na picha, jaribu kutumia muktadha wa sentensi kubainisha maana ya maneno mapya (jaza nafasi zilizo wazi kwenye kisanduku).

Toku =

Gotuki =

?

Unadhani maneno haya yana maana gani kwa Kiswahili?

1. Toku: _____

2. Gotuki: _____

3. Kukiki: _____

4. Bilabu: _____

5. Wawati: _____

UTANGULIZI

WAAMBIE WALIMU:

“Sasa tumemaliza, tafadhali soma maswali peke yako na fikiria kuhusu majibu. Jadili majibu yako na mwenzako wako. Halafu utashirikisha mawazo yako kwenye kikundi.”

Ikiwa walimu wana matatizo, hapa kuna majibu yanayopendekezwa:

1. tulitumia muktadha wa sentensi kubainisha maana za maneno
2. tulitumia picha kubaini maana za maneno
3. tulitumia maarifa yetu ya awali kuhusu dhana kama vile ‘sauti za herufi’ na ‘sarufi’ (kutumia ‘ku’ kwa vitenzi), maarifa ya awali

DHANA KUU

WAAMBIE WALIMU:

“Sasa tutasoma maudhui muhimu. Tutasoma kwa sauti matini kwa kupokezana.

Baada ya mwalimu wa kwanza kusoma aya ya kwanza, atamwita mwalimu mwingine kwa jina ili asome aya inayofuata.

Wakati wa kusoma weka alama zifuatazo kwenye matini unayosoma.

Weka alama ya mshangao (!) Kwenye wazo ambalo unadhani ni muhimu.

Weka alama ya kuuliza (?) Kuonesha kutokukubaliana na dhana hiyo.

Weka alama ya mduara (O) kuonesha kuwa dhana hiyo ni mpya kwako.”

UTANGULIZI

FIKIRI –JOZISHA- SHIRIKISHANA (DAKIKA 5)

Baada ya mratibu kusoma maneno yote, jadili maswali yafuatayo ukiwa na mwenzako:

1. Mbinu gani ulizitumia kubainisha maana ya maneno mageni?

DHANA KUU

UMUHIMU WAKUKUZA MSAMIATI (DAKIKA 35)

1. Mwalimu mmoja aanze kusoma kwa sauti. Baada ya kukamilisha sehemu (kwa mfano, aya au maelezo) amwite mwalimu mwingine kwa jina asome sehemu inayofuata.
2. Wakati unaposoma zingatia alama zifuatazo:
    - Weka alama ya mshangao (!) katika sehemu ambayo unaona ni muhimu.
    - Weka alama ya kuuliza (?) katika sehemu ambayo huelewi au hukubaliani nayo.
    - Weka mduara katika (o) maneno ambayo ni mapya.

Moduli hii inahusu ukuzaji wa msamiati, ambao ni mchakato kwa wanafunzi wanajifunza kutumia maneno mapya. **Kuna aina nne za msamiati:**

1. **Msamiati wa kusikiliza** – maneno ambayo tunayaelewa wakati wengine wanapoongea.
2. **Msamiati wa kuongea** – maneno tunayoyajua tukiwa tunaongea na wengine.
3. **Msamiati wa kusoma** – maneno tunayoyajua tukiyaona yameandikwa.
4. **Msamiati wa kuandika** – Maneno tunayoyajua tunapotumia maandishi.

DHANA KUU

WAAMBIE WALIMU:

“Tunaendelea kusoma matini kwa sauti na kwa kupokezana.”

DHANA KUU

Msamiati wa kusikiliza na kuongea ni kundi la maneno ambalo wanafunzi wanalibainisha na kuelewa maana yake wanaposikia au kusema. Tambua kuwa wanafunzi wanaweza kujua neno kwa kulitamka, lakini wasibaini ikiwa wataliona limeandikwa. Msamiati wa kusoma na kuandika ni kundi la maneno ambayo wanafunzi wanabaini na kuelewa maana zake wanapoyasoma au kuyaandika katika mfumo wa maandishi. Kumbuka kuwa wanafunzi wanaweza kubaini neno lililoandikwa, lakini kama hawajui maana yake, neno hilo siyo sehemu ya msamiati wao wa kusoma na kuandika.

Mwanafunzi anayekutana na neno geni katika chapisho anaweza kutumia ujuzi wa foniki kuhusianisha neno na kulisoma kwa sauti. Kama neno hilo ni msamiati wa kutamka wa mwanafunzi, mwanafunzi atakuwa na uwezo wa kuelewa unamaanisha nini. Kama neno halimo kwenye msamiati wa kutamka, mwanafunzi atapaswa kubainisha maana ya neno hilo kwa kutumia njia nyingine. Moduli hii ina mbinu ambazo sinaweza kumsaidia mwalimu KUFUNDISHA mwanafunzi aweze kubaini maana ya maneno mapya.

1. Baini aina ya msamiati

Mwalimu anapojiandaa KUFUNDISHA msamiatianapaswa kufikiri aina ya msamiati ili kubaini mbinu ambayo itaeleza vizuri maana ya msamiati huo. Kwa mfano, "paka" au "kimbia" ni kitu au kitendo? Au "njaa" au 'amani" ni wazo au dhana? Hapa chini kuna mifano ya msamiati wa aina hii:

	Kitu au Kitendo	Wazo au Dhana
Darasa la. 1	ng'ombe kimbia mti	saidia penda furahi
Darasa la. 2	ndoo shule andika	choka kosa amani
Darasa la. 3	simu hospitali lia	mafanikio ajali njaa

Kujua aina ya msamiati unaotaka KUFUNDISHA kutakusaidia kuamua njia bora ya KUFUNDISHA maana yake. Msamiati unaweza kuwa katika makundi matatu ambayo ni: 1) dhana, 2) vitendo, 3) vitu. Msamiati ambo ni kitu au kitendo ni rahisi kuufundisha kwa sababu unaweza kufanyia vitendo au kutolea mifano. Msamiati ambo ni wazo au dhana unaweza kufundishwa kwa vitendo; hata hivyo, msamiati huu mara nyingi huhitaji mbinu tofauti kuwafanya wanafunzi waelewe maana zake. Hapa chini kuna mbinu muhimu kwa ajili ya kufundishia aina zote za msamiati. Tafadhali kumbuka kwamba ni muhimu mara nyingi kutumia mbinu zaidi ya moja ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wanaelewa maana yake.

Mbinu za kufundishia msamiati ambao ni vitu au vitendo

Mbinu	Maelekezo	Mfano
Onesha/chora picha	Onesha au chora picha kuelezea maana ya msamiati.	Katika zoezi la kuchangamsha, maana ya "toku" ilitolewa kwa njia ya picha ya shule.
Igizo	Igiza maana ya msamiati.	Jifanye umelala kuelezea maana ya neno "lala".
Onesha vitu halisi	au bainisha vitu vilivyomo ndani ya darasa ambavyo vinaelezea maana ya msamiati mapya.	Leta matunda kutoka sokoni wakati unafundisha majina ya matunda tofauti.

DHANA KUU

WAAMBIE WALIMU:

“Tunaendelea kusoma matini kwa sauti na kwa kupokezana.”

DHANA KUU

Mbinu za kufundishia msamiati ambao ni wazo au dhana

Mbinu	Maelekezo	Mfano
Onesha picha ya kitu halisi	Onesha au chora picha kueleza maana ya msamiati.	Chora picha au onesha kidole kwa mtu aliyetabasamu kuonesha maana ya 'kufurahi'.
Igizo	Igiza maana ya msamiati.	Sugua tumbo lako kuonesha maana ya 'njaa'.
Maelekezo	Eleza maana ya msamiati na/au kinyume chake.	Elezea 'kuchoka' kama "kutaka kupumzika' na/au 'kutokuwa na nguvu'.
Weka mifano	Tumia vitu au uzoefu wa wanafunzi katika kueleza maana ya msamiati.	Onesha maana ya 'ajali' kwa kuorodhesha mifano ya ajali kama vile kuruka na kuanguka, au kudondosha kikombe ili kipasuke.
Weka visawe	Tumia msamiati yenye maanaile ile.	Onesha maana ya 'kufahamu' kuwa sawa na 'kujua' na 'kuelewa'.
Eleza kinyume	Elezea kitu ambacho kinamaanisha kinyume kuonesha maana ya msamiati.	Elezea 'amani' kama kinyume cha 'vita'.
Eleza maana	Tumia kamusi kueleza maana ya msamiati moja kwa moja.	Eleza maana ya 'mafanikio' kama jambo linalofanywa kwa kufanikishwa.
Fasiri kwa lugha ya asili ya wanafunzi (kama inatumika)	Tumia lugha ambayo wanafunzi wanaielewa zaidi ili kuwafahamisha maana ya msamiati.	Tafsiri 'kiti' (Kiswahili) kuwa 'lisumbi' (Kisukuma). Wekea alama kwenye vitu vilivyopo darasani kwa maneno ya Kiswahili.

2. Fundisha msamiati kwa kuzingatia muktadha husika

KUFUNDISHA maneno mapya ambayo yanaendana na mada kunamsaidia mwanafunzi kukumbuka na kuyatambua haraka zaidi. Kwa mfano, msamiati kiini wa "shule" unaweza kujumuisha msamiati ambayo ni vitu/vitendo kama vile: dawati, mwalimu, soma. Vilevile msamiati ambayo ni wazo/dhana kama vile: mafanikio, elimu, giza.

3. KUFUNDISHA msamiati mpya kabla ya kusoma

Moja ya njia muhimu ya kuwasaidia wanafunzi namna ya kujifunza msamiati ni kuwafundisha maneno mageni ambayo yanapatikana kwenye kitabu kabla ya kuyasoma. Kwa mfano, kabla ya kusoma andiko kwa sauti darasani au kuwafungulia ukurasa mpya kwenye andiko, pitia andiko na bainisha maneno ambayo unafikiria wanafunzi hawatayafahamu. Halafu, kabla ya kuanza kusoma rasmi kifungu, pitia maneno pamoja na wanafunzi, neno moja baada ya lingine, tumia mbinu kutoka sehemu ya kwanza KUFUNDISHA maana ya maneno hayo. Onesha kidole kwenye neno ili wanafunzi wakumbuke maana yake wakiliona neno kwenye andiko.

4. Tumia muktadha wa neno kubainisha maana yake

Wanafunzi wanaweza kutumia msamiati mwengine kwenye sentensi au mifano kubainisha maana za msamiati mgeni. Wakaiti wa zoezi la kuchangamsha ulifanya yatuatayo: 1) ulibainisha mada iliyoko kwenye matini (shule na kujifunza kusoma); na 2) ulitumia stadi ya foniki kubainisha maana ya msamiati.. Wanafunzi lazima wafundishwe kutafuta na kutumia vidokezo vilivyozunguka mambo yaliyomo kweye kitabu ili kubainisha maana ya maneno mageni. Kusoma vitabu kwa nguvu darasani ni njia nzuri ya kufanya jambo hili. Kama ukikutana na neno geni na ambalo hukulifundisha kabla ya kulisoma, uliza maswali kuhusu mfano na nini kinachotokea kwenye hadith ili kuwasaidia wanafunzi kuthibitisha maana ya neno.

DHANA KUU

WAAMBIE WALIMU:

“Tunaendelea kusoma matini kwa sauti na kwa kupokezana.”

WAAMBIE WALIMU:

“Sasa kila mwalimu anaweza kushirikisha wenzake kitu ambacho ameona ni muhimu, hakieleweki au ni kipya. Halafu tunaweza kujadili mbinu ambazo tunadhani zilikuwa muhimu sana katika kukuza msamiati wa wanafunzi.”

DHANA KUU

5. Rudia yatokanayo na msamiati mpya
Utafiti unaonesha kuwa wanafunzi wanahitaji kuona na kuelewa maana ya neno jipya mara saba katika mazingira tofauti kabla ya kujifunza neno hilo. Uzingatiaji wa fursa nyingi za kutumia neno jipya katika mfumo wake wa kuandikwa na kutamkwa, unawasaidia wanafunzi kukuza uelewa wao kuhusu maneno hayo. Hapa kuna hatua saba za KUFUNDISHA kwa ufanisi na kuhakikisha wanafunzi wanayafahamu maneno mapya:

a) **Hatua ya kwanza:** Eleza maana ya neno jipya kwa kutumia mbinu zilizoorodheshwa kwenye sehemu ya 1. Hakikisha wanafunzi wanaona neno lililoandikwa ili kujenga uwezo wao juu ya msamiati uliochapishwa pia.
b) **Hatua ya pili:** Tumia neno mara 2 – 3 kwenye sentensi tofauti. Pia andika sentensi hizo
c) **Hatua ya tatu:** Waulize wanafunzi kufafanua tena au kuelezea neno jipya kwa namna wanayojua. Hii inaweza kufanywa kwa kutamka, kwa kuandika, kwa kuchora au kwa igizo.
d) **Hatua ya nne:** Tamka, andika au onesha kwa kidole kwenye neno kwa mara nyingine katika mazingira tofauti (Tumia neno katika mjadala, liandike katika ujumbe wa asubuhi, lioneshe kwenye hadithi au kitabu).
e) **Hatua ya tano:** Waambie wanafunzi wajitolee ukurasa wa mwisho wa madaftari yao kwa ajili ya msamiati mpya. Watake waandike maneno mapya na maana za maneno hayo (hii ni sahihi zaidi kwa wanafunzi wa darasa la 2 – 3 na kuendelea)
f) **Hatua ya sita:** Tengeneza "Ukuta wa Maneno" ambayo ni sehemu ya ukuta wa darasa ambapo utaweka neno kwenye kadi ya neno kwa kila neno jipya ambalo limeletwa (maelekezo ya namna ya kutengeneza ukuta wa neno yako kwenye Kivunge cha Kufundishia kwenye sehemu ya moduli hii)
g) **Hatua ya saba:** Waruhusu wanafunzi wafanye mchezo kupitia na kufanyia mazoezi msamiati mpya (michezo miwili imewekwa kwenye mpango kazi wa moduli hii)

Kwa ujumla, kumbuka kwamba sehemu ya msamiati wa kufundishia inaamua maneno yapi yataletwa au yatafundishwa wakati wa maelekezo ya msamiati. Ili kufanya hili:

1. Bainisha maneno ambayo wanafunzi hawayafahamu.
2. Bainisha maneno ambayo wanafunzi watakutana nayo mara nyingi.
3. Bainisha maneno muhimu zaidi kwenye andiko au kifungu cha maneno ambayo utakuwa ukifundisha.
4. Bainisha maneno ambayo wanafunzi hawawezi kuyatambua wakitakiwa kufanya hivyo peke yao.

FIKIRI – JOZISHA– SHIRIKISHANA (DAKIKA 10)

Jibu maswali yafuatayo ukiwa na mwenzako. Halafu tutashirikishana majibu yetu pamoja na kikundi chote.

1. Maudhui gani umewekea alama ya mshangao (!)?
2. Maudhui gani umewekea alama ya kuuliza (?)?
3. Maudhui gani umezungushia alama ya mduara?
4. Mbinu zipi ni muhimu sana kusaidia kukuza uwezo wa mwanafunzi kutamka na kusoma msamiati uliochapishwa?

ZOEZI

WAAMBIE WALIMU:

“Sasa ni zamu yako kufanya mazoezi ya mpango wa KUFUNDISHA msamiati. Sasa tusome maelekezo pamoja na kisha tutakaa wawiliwawili kukamilisha chati na kufanya igizo.”

(Tembea kuzunguka darasa na angalia namna walimu wanavyofanya. Baada ya dakika 25, wakumbushe walimu kuwa wamebakiza dakika tano tu kumaliza).

ZOEZI

IGIZO (DAKIKA 30)

Sasa ni zamu yako kufanya mazoezi ya KUFUNDISHA msamiati mpya pamoja na mwenzako. Hapa chini kuna orodha ya maneno. Wewe pamoja na mwenzako lazima muamue nani atafundisha maneno miwili ya kwanza na nani atafundisha maneno miwili ya mwisho. Mtu mmoja ataigiza kama mwalimu kwa maneno matatu ya mwanzo na mwingine atakuwa mwanafunzi. Halafu mtabadilishana. Pamoja na mwenzako, bainisha hatua nne ambazo utatumia KUFUNDISHA kila neno. Mbinu ya kwanza imefanywa kwa ajili yako kama mfano. Mara ukishamaliza kujaza chati, igiza hatua ya 1 – 3 na mwenzako (na hatua ya 4 kama inatumika).

Msamiati	**Makundi ya msamiati**	**Hatua ya 1: Ni mbinu ipi/zipi utafundishia maana ya neno?**	**Hatua ya 2: Namna gani utatumia neno katika sentensi 2 – 3 tofauti?**	**Hatua ya 3: Ni namna gani utafanya ili wanafunzi waelezee neno kwa namna yao? (Kwa kutamka, kuandika, kuchora, kuigiza)**	**Hatua ya 4: Ni namna gani utatamka, utaandika au kuonesha neno kwa mara nyingine baadaye?**
Leo	Wazo/ dhana	Maelekezo: Leo inare-jelea siku ya leo. SASA HIVI. Siyo kesho au jana. Onesha kitu: Onesha tarehe ya leo kwenye kalenda.	Leo, nimekuja shuleni. - Leo najisikia furaha. - Leo ni tarehe 12 Juni 2015.	Waelekeze wanafunzi wafanye kazi wakiwa wawiliwawili kufikiri juu ya sentensi nyingine zinazotumia neno 'leo'. Halafu waambie wazi-tamke.	- Andika na tamka neno katika ujumbe wa asubuhi. - Onesha kidole kwenye neno katika ujumbe na hadithi
Simu					
Huzuni					
Cheza					
Bora					

ZOEZI

WAAMBIE WALIMU:

“Sasa umemaliza kumfundisha mwenzako msamiati, hebu tujibu maswali haya ya mjadala kwa kuongea.”

ZOEZI

JADILIANA KATIKA KIKUNDI KIKUBWA (DAKIKA 10)

Baada ya kumaliza igizo lenu, rudini kwenye kikundi na kujadiliana juu ya maswali yafuatayo:

1. Shirikisha mbinu ambazo ulitumia kwa kila neno (hatua ya 1)
2. Shirikisha namna utakavyowafanya wanafunzi waelezee kila neno kwa namna yao (Hatua ya 3)
3. Ni namna gani ufundishaji wa maneno mapya kwa njia hizi unaweza kutosheleza masomo yako ya kila siku?

KUPANGA MKAKATI

WAAMBIE WALIMU:

“Sasa tutapanga vipindi vyetu vya kusoma na kuandika.Tutasoma maelekezo kwa pamoja na kwa sauti. Baada ya mwalimu wa kwanza kusoma sehemu, anaweza kuita jina la mwalimu mwingine ili asome sehemu inayofuata.”

KUPANGA MKAKATI

KUAANDAA KIPINDI CHA "KUSOMA NA KUANDIKA" (DAKIKA 20)

Ili kukuza uwezo wa wanafunzi kusoma, ni muhimu sana kwamba aweze kufanya mazoezi juu ya mbinu mpya za kusoma na kuandika alizosoma kutoka kwenye Mafunzo ya Walimu Kazini.

Kurasa zifuatazo zinajumuisha masomo ya jumla yanayoelekeza shughuli ambazo unaweza kujaribu wakati wa kipindi chako cha kusoma na kuandika (au unaweza pia kujaribu wakati wa kipindi chako cha kawaida cha Kiswahili). Pamoja na mwenzako:

1. Soma kwenye mpango wa masomo.
2. Jaza nafasi zilizo wazi mahali panapohitaji hivyo.
3. Jaribu masomo wakati wa kipindi cha kusoma na kuandika.

MWONGOZO WA SOMO LA KWANZA: KUFUNDISHA Msamiati Mpya
HATUA ZA KUFUNDISHA

HATUA	SHUGHULI ZA KUFUNDISHIA
MAANDALIZI	1. Kabla ya siku ya kipindi, kusanya orodha ya maneno ambayo ni msamiati ambayo hujawahi kuyafundisha kwa kiwango chako. Haya ni maneno ambayo unaweza kuyapata kwenye mtaala wa Kiswahili, lakini unaweza pia kuongeza maneno yoyote ya ziada ambayo unafikiri yanaendana na ngazi yako. Hapa chini kuna mfano wa maneno ambayo yamechukuliwa kwenye mtaala wa Kiswahili wa kila ngazi: **Kipengele cha maandalizi kiwe peka yake kwani hakiko katika hatua za somo.**

Maneno kwa Darasa la 1	Maneno kwa Darasa la 2	Maneno kwa Darasa la 3
Mama	Kofia	Sokoni
Baba	Koti	Singizia
Mimi	Viatu	Jenga
Jina	Vijiko	Katili
Kitabu	Wanyama	Ulimbo
Kalamu	Wadudu	Huruma
Meza	Baridi	Kalenda
Vikombe	Mrefu	Mizani

KUPANGA MKAKATI

(Zunguka na uliza ikiwa walimu wanahitaji msaada)

KUPANGA MKAKATI

<table>
<tr><th>HATUA</th><th>SHUGHULI ZA KUFUNDISHIA</th></tr>
<tr><td>MAAN DALIZI</td><td>2. Chukua moja ya maneno kwa ajili ya kuwekeza umakini katika somo hili.
3. Halafu jaza kielelezo kilichoko hapa chini kupanga hatua tofauti kwa ajili ya KUFUNDISHA neno hili (weka umakini pia kwa wanafunzi ambao wanajifunza Kiswahili na wanajaribu kufasiri neno kwenda kwenye lugha yao ya asili).
<table>
<tr><td>Neno:</td><td></td></tr>
<tr><td>Aina ya (kitu/kitenzi au wazo/dhana)</td><td></td></tr>
<tr><td>Hatua ya 1: Ni mbinu gani utaitumia KUFUNDISHA maana ya neno?</td><td></td></tr>
<tr><td>Hatua ya 2: Namna gani utatumia neno kwenye sentensi 2 – 3 tofauti?</td><td></td></tr>
<tr><td>Hatua ya 3: Namna gani utawafanya wanafunzi kueleza neno kwa namna yao? (kwa kutamka, kuandika, kuchora au kuigiza)</td><td></td></tr>
<tr><td>Hatua ya 4: Ni namna gani utatamka, kuandika au kuonesha kidole kwenye neno siku zijazo?</td><td></td></tr>
<tr><td>Hatua ya 5: Ni namna gani utapenda wanafunzi waandike neno hili na maana yake kwenye madaftari yao?</td><td></td></tr>
<tr><td>Hatua ya 6: Je, umetengeneza kadi neno kwa hili neno na kuliweka kwenye ‘Ukuta wa Kadi’?</td><td></td></tr>
<tr><td>Hatua ya 7: Ni mbinu gani utaitumia kuwafanya wanafunzi washiriki na kupitia neno hili?</td><td></td></tr>
</table></td></tr>
<tr><td>UTANG ULIZI</td><td>1. Waambie wanafunzi kwamba leo watasoma neno jipya (taja neon hilo)
Uliza ikiwa kuna mwanafunzi yeyote anafahamu maana ya neno hilo. Kama wanafunzi wachache wanafahamu maana yake, tumia maelezo yao kuongeza mbinu ambayo utaitumia KUFUNDISHA darasa zima.</td></tr>
<tr><td>KU-JENGA UMA-HIRI</td><td>2. Anza na hatua ya 1 kutoka kwenye chati hiyo hapo juu: tumia mbinu ambayo umeichagua kufundishia maana ya neno
3. Hatua ya 2: tumia neno jipya walau mara 2 – 3 kwenye sentensi tofauti. Tamka sentensi hizi na ziandike kwenye ubao.
4. Hakikisha wanafunzi wote wanaelewa maana ya neno.</td></tr>
</table>

KUPANGA MKAKATI

(Zunguka na uliza ikiwa walimu wanahitaji msaada)

KUPANGA MKAKATI

HATUA	SHUGHULI ZA KUFUNDISHIA
KUTUMIA UMAHIRI	5. Hatua ya 3: waambie wanafunzi waelezee neno kwa namna yao wenyewe (ama kwa kutamka, kuandika, kuigiza – au kwa namna hizi zote) 6. Hatua ya 4: Waambie wanafunzi kwamba utasema, utaandika na kuonesha neno kwa kidole hapo baadaye. Waambie na wao wafanye hivyo hivyo.
KUTUMIA UMAHIRI	7. Hatua ya 5: Waambie wanafunzi waandike neno hili na maana yake kwenye madaftari yao. Unaweza kuwapa mfano kwenye ubao. 8. Hatua ya 6: Weka kadi neno kwa hili neno kwenye 'Ukuta wa Neno' mbele ya wanafunzi 9. Hatua ya 7: Waambie wanafunzi wafanyie mazoezi na wapitie neno hili wakiwa wawiliwawili
TATHMINI	10. Katika somo hili, unaweza kueleza kama wanafunzi wameelewa maana ya neno ikiwa wanaweza kulieleza kwa usahihi kwa maneno yao wenyewe, au ikiwa wanaweza kufikiri njia mpya za kulitumia kwenye sentensi. 11. Katika somo la mbele, baada ya kuwa umefundisha maneno mapya 4 – 5, unaweza kufanya tathmini ikiwa wanafunzi wanakumbuka maana ya maneno haya kwa kuyatamka kuelezea maana ya maneno na waambie wanafunzi waandike maneno kwenye madaftari yao 12. Wakati unasahihisha madaftari, angalia maneno gani wanafunzi wanatatizwa nayo na rudia kufundisha kwa kutumia mifano mipya au mbinu mpya.

Tathmini ya Ufundishaji: _____

Tathmini ya Ujifunzaji: _____

Maoni: _____

MWONGOZO WA SOMO LA PILI: Kufanyia Mazoezi Msamiati Mpya
HATUA ZA KUFUNDISHA

HATUA	SHUGHULI ZA KUFUNDISHIA
MAANDALIZI	1. Kabla ya siku ya somo, kusanya orodha ya walau maneno mapya 8 -10 ambayo umewafundisha wanafunzi katika miezi michache iliyopita. 2. Huu ni mchezo ambao utawasaidia wanafunzi kufanya mazoezi na kukumbuka maana ya maneno haya (hatua ya 7 kwenye mpango wa somo uliopita) Sio sehemu ya hatua za somo
UTANGULIZI	3. Waambie wanafunzi kwamba watafanyia mazoezi msamiati mpya kwa kucheza mchezo 4. Utaligawa darasa katika timu mbili na muombe mwanafunzi atakayejitolea kubashiri neno 5. Timu mbili zitatoa 'vidokezo' kwa mwanafunzi anayejitolea kuhusu maana ya neno (bila kusema neno!). Anayejitolea naye atapaswa kubashiri hilo neno ni lipi. 6. Timu ambayo imetoa kidokezo ambacho kimepelekea anayejitolea pamoja na wanafunzi kubashiri neno sahihi, litakuwa limepata alama. 7. Mwambie anayejitolea aanze na waambie wanafunzi wasimame mbele ya darasa wakiwaangalia wanafunzi (migongo yao ikiwa inaangaliana na ubao) 8. Ligawe darasa zima kwenye makundi mawili.

KUPANGA MKAKATI

(Zunguka na uliza ikiwa walimu wanahitaji msaada)

KUPANGA MKAKATI

HATUA	SHUGHULI ZA KUFUNDISHIA
KUJENGA UMAHIRI	1. Andika neno moja la msamiati kwenye ubao. Linapaswa kuwa na ukubwa wa kutosha kwa kila mwanafunzi kuona, lakini usiruhusu anayejitolea kuliona. Hakikisha wanafunzi wengine hawasemi neno kwa sauti. 2. Karibisha mwanafunzi kutoka kwenye timu moja atoe kidokezo ili kumsaidia anayejitolea kubashiri neno husika. **Mfano, neno: "jenga"** Wanafunzi wanaweza kujaribu kuigiza neno Wanafunzi wanaweza kusema, "Hiki ndicho unafanya kwenye nyumba au jengo" Wanafunzi wanaweza kusema, 'Ni pale ambapo jengo ni dogo na halafu linamalizika" 3. Wakati mwanafunzi anayejitolea analifahamu neno, ananyoosha mkono wake na kubashiri. 4. Baada ya anayejitolea kubashiri neno kwa usahihi, toa alama kwa timu ambayo imetoa kidokezo cha mwisho. 5. Halafu ita mwanafunzi mwingine kuja mbele ya darasa na rudia shughuli kwa neno jipya.
KUTUMIA UMAHIRI	1. Cheza mchezo huu hadi maneno yote kwenye orodha yako yawe yametumika. 2. Wagawe wanafunzi wawiliwawili (au makundi madogo ya wanafunzi 3 – 4). Liambie kundi lichague mwanafunzi mmoja kuanza 3. Wanafunzi wote isipokuwa aliyechaguliwa katika kila kundi watapaswa kufumba macho yao. Wote wanapofumba macho, andika neno kwenye ubao ambalo wanafunzi waliochaguliwa watapaswa kuliigiza. 4. Wewe pamoja na wanafunzi hampaswi kulitamka neno kwa sauti, lakini kwa kuona hakikisha kwamba wanafunzi hawa wote wanaliona neno vizuri. 5. Sema, 'Ndiyo, kila mmoja afumbue macho yake! Sasa, mwenzako wako ataigiza neno la siri. Angalia kama unaweza kulibashiri!" 6. Waambie wanafunzi waliochaguliwa kuigiza neno au kutoa 'vidokezo' kuhusu neno hilo. 7. Wanafunzi watapaswa kuigiza neno hadi mwenzako wao abashiri msamiati sahihi wa neno husika 8. Mara tu kundi likishabashiri kwa usahihi, watachagua mwanafunzi mwingine kuigiza na kurudia mchezo huu.
TATHMINI	9. Tembea kuzunguka darasani wakati wa mchezo na tilia mkazo kwa wanafunzi ambao wanaelewa polepole maneno na yatambue maneno ambayo wanatatizwa nayo. 10. Rudia kufundisha maneno kwa wanafunzi wanaotatizwa kwa kutumia mifano mipya na/au mbinu mpya.

Tathmini ya Ufundishaji: _____

Tathmini ya Ujifunzaji: _____

Maoni: _____

UTENGENEZAJI WA ZANA ZA KUFUNDISHA

WAAMBIE WALIMU:

“Sasa tutaanza sehemu ya utengenezaji wa vifaa vya kufundishia kwa ajili ya moduli hii. Baada ya mwalimu wa kwanza kusoma sehemu ya kwanza, anaweza kuita jina la mwalimu mwingine kusoma sehemu inayofuatia.”

UTENGENEZAJI WA ZANA ZA KUFUNDISHA

KUTENGENEZA UKUTA WA MANENO (DAKIKA 30)

Wanafunzi wanapojifunza maneno mapya, ni muhimu kwamba waone na kusikia maneno haya mara nyingi na kwa namna tofauti. Namna moja ya kuwafanya wanafunzi wafikirie kuhusu msamiati ni kuweka maneno hayo kwenye Ukuta wa Neno. Ukuta wa Neno ni sehemu ya ukuta wa darasani kwako ambao umeandaliwa kwa ajili ya maneno ya msamiati na ni njia moja yenye ufanisi katika kutengeneza maneno yaliyochapishwa na yanayoonekana vizuri kwa kila mwanafunzi darasani. Fikiri kuhusu Ukuta wa Neno kama sehemu ya kudumu na inayoendelea katika darasa – wakati wanafunzi wanajifunza maneno mapya ambayo utayaweka kwenye Ukuta wa Neno ili, mwisho wa mwaka, ukuta huo uwe uthibitisho unaoonekana kwamba kumekuwa na ukuaji wa kutosha wa msamiati kwa wanafunzi wako! Leo, utafanya seti moja ya Kadi Neno. Kutengeneza Kadi Neno zako, utahitaji vifaa vifuatavyo:

VIFAA VYA KADI YA PICHA

√ Viweka alama au mkaa
√ Manila kadi za A4 za rangi tofauti (karatasi 6-8 kwa mtu mmoja)
√ Orodha ya majina 10 ambayo umekwishayafundisha au unataraji kuyafundisha kwa kiwango cha darasa unalofundisha.
√ Gundi ya karatasi
√ Utando fomeka (kama upo)

HATUA YA 1:
Tengeneza jina la Ukuta wa Maneno Juu ya kipande kimoja cha karatasi ya A4, andika maneno "UKUTA WA NENO" kwa ukubwa wa kutosha iwezekanavyo. Alama hii ya kichwa cha habari itawaonesha wanafunzi wapi waangalie kwa ajili ya maneno mapya ambayo wamesoma.

HATUA YA 2:
Chagua maneno kwa ajili ya Ukuta wa Maneno
Unaweza kutumia orodha ya maneno ambayo umekuja nayo (ya maneno uliyofundisha au utakayofundisha kwa kiwango cha darasa lako). Tengeneza orodha ya maneno 10 kwa ujumla.

HATUA YA 3:
Kunja karatasi na kata kadi Kunja karatasi yako ya A4 kwa nusu. Kwa maneno mafupi, kunja karatasi kwa upana. Halafu kata kwa kufuata mstari kutengeneza kadi mbili kwa maneno mawili mafupi. Kwa maneno marefu, kunja karatasi kwa urefu. Halafu kata kwa kufuata mstari kwa maneno mawili marefu. Fanya hivi kwa maneno yote uliyochagua.

UTENGENEZAJI WA ZANA ZA KUFUNDISHA

WAAMBIE WALIMU:

“Tunaendelea kusoma matini kwa sauti na kwa kupokezana.”

UTENGENEZAJI WA ZANA ZA KUFUNDISHA

HATUA YA 4:
Andika neno moja kwa kila kadi Tumia viweka alama, vichorezi au mkaa, andika neno la msamiati mmoja kwa kila kadi. Usitumie mviringo na fanya herufi ziwe kubwa na zinazoonekana zaidi ili wanafunzi waliokaa nyuma katika darasa waweze kuziona kirahisi.

HATUA YA 5:
Kama una Kivunge cha Vifaa vya Kufundishia cha EQUIP-Tanzania, fomeka sehemu yenye jina la ukurasa na kadi neno kwenye "Ukuta wa Neno" Rejea kwenye moduli ya 7 kwa ajili ya maelekezo ya namna ya kufomeka.

HATUA YA 6:
Tumia gundi ya karatasi kubandika kadi za maneno kwenye ukuta Chagua sehemu ya ukuta ambayo inaweza kuonekana vizuri kwa wanafunzi wote. Tumia mkanda uliofunikwa kuchomeka "Ukuta wa Neno" juu ya ukuta kisha chomeka kadi maneno chini yake.



UFUATILIAJI

Baada ya kumaliza moduli hii, Mratibu Elimu wa Kata, Ofisa Elimu wa Wilaya na Mkaguzi Elimu wa Wilaya watafuatilia kuona namna unavyotumia mbinu za moduli hii darasani kwako. Wakati wa ufuatiliaji huu, ni vema ukawa na uwezo wa kuonesha mambo yafuatao:

a) Onesha mbinu 2 – 3 kwa kufundishia maneno ambayo ni vitu/vitenzi
b) Onesha mbinu 2 – 3 kwa kufundishia maneno ambayo ni mawazo/dhana
c) Onesha kadi maneno ambazo umetengeneza
d) Onesha namna ulivyotumia mpango wa somo kutoka kwenye moduli hii katika darasa lako.

MWISHO

WAAMBIE WALIMU:

"Walimu, tumefika mwisho wa moduli yetu, tumia dakika kumi kutafakari somo letu la leo. Jaza fomu kurekodi tathmini yako ya moduli. Baada ya kukamilisha chomoa ukurasa huo unipatie. Tafadhali uwe mkweli katika majibu yako kwa sababu yatasaidia kuboresha Mafunzo ya Walimu Kazini ngazi ya shule hapo baadaye."

Kusanya fomu za tathmini zilizokamilishwa na walimu na uwe nazo wakati wa mkutano mwingine katika kundi la kata.

Wakati walimu wanaendelea kujaza fomu za tathmini, tafadhali tafakari kwa ujumla juu ya mafanikio na changamoto zilizojitokeza katika kipindi cha siku hiyo na jaza visanduku vinavyofuata. Haya utaweza kuyajadili pamoja na Timu ya Wilaya ya Mafunzo Walimu Kazini na Waratibu wengine wa Mafunzo Walimu Kazini wa mkutano unaofuata katika kundi la kata.

MAFANIKO YA JUMLA YA KIPINDI HIKI:	CHANGAMOTO ZA JUMLA ZA KIPINDI HIKI:

Shule: _____ **Wilaya:** _____ **Mkoa:**_____

Tafakuri za Moduli # _____ **Mada ya Moduli:** _____

Idadi ya walimu walioshiriki : _____ **Mwalimu Mkuu alishiriki : Ndiyo/Hapana**

MWISHO

MWISHO (DAKIKA 10)

Binafsi jaza fomu ifuatayo kuweka rekodi ya tathmini ya moduli ya leo. Baada ya kukamilisha, chomoa ukurasa huu na umpe Mratibu wako. Tafadhali uwe mkweli kwa vile mrejesho wako utasaidia kuboresha Mafunzo ya Walimu Kazini ngazi ya shule hapo baadaye.

JEDWALI LA KUTATHMINI			
Alama 0: Sikubaliani kabisa na usemi huu	**Alama 1: Kwa kiasi Sikubaliani** na usemi huu	**Alama 2: Nakubaliana kwa kiasi** na usemi huu	**Alama 3: Nakubaliana Kabisa** na usemi huu

FOMU YA TATHMINI

Shule: _____ **Wilaya:** _____ **Mkoa:**_____

Tathmini ya Moduli: _____ **Mada ya Moduli:** _____

Idadi ya walimu walioshiriki: _____ **Mwalimu Mkuu alishiriki: Ndiyo/Hapana**

Mratibu alikuwepo kuwezesha: Ndiyo/Hapana

Soma semi zifuatazo kisha weka alama ya vema katika kisanduku husika kuonesha jibu lako:	**0**	**1**	**2**	**3**
1. Dhana kuu ya moduli ya leo ilikuwa inaeleweka.				
2. Moduli hii ina mikakati mingi mizuri na yenye manufaa ambayo nitaitumia darasani kwangu.				
3. Muda uliotumika kukamilisha moduli hii unafaa. Sikuhisi kwamba ni muda mrefu sana.				
4. Moduli hii iliibua mjadala wa kufurahisha na tafakuri ya hali ya juu sana.				
5. Violezo vya kipindi cha kusoma na kuandika vilisaidia sana. Natarajia vitakuwa rahisi kuvitumia ndani ya darasa langu.				
6. Zana tulizotengeneza leo zitakuwa za manufaa sana (kama inahusika).				
7. Mratibu amejiandaa kwa kipindi – amesoma vizuri moduli na ameandaa vifaa vyote vya kufundishia.				
8. Mratibu anasimamia vizuri majadiliano – anajua jinsi ya kuwafanya watu wajieleze na namna ya kupata majibu.				
9. Mratibu anajua namna ya kusimamia makundi – anahakikisha kuwa walimu wanatoa ushirikiano, wanashirikiana na wana hamasika.				
10. Mratibu anajua jinsi ya kuwahamasisha walimu – anafuatilia kujua waliokosa vipindi au kuchelewa na kutukumbusha kwanini Mafunzo ya Walimu Kazini ni muhimu kwetu.				